GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

# Mapenzi Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

**JUZU NO.** 240 **Dh.Qa'dah-Dh.Hijjah** 1445 **AH** **Juni–** 2024 **Ihsan** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

# Kuzingatia Ucha-Mungu kwenye kila kitendo ni jukumu letu.

## Khalifa wetu wa Tano Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. alisema akitoa hotuba ya siku ya Dhabihu tar.23 Julai 2021

Leo ni Eid ul-Qurban, ambayo pia tunaiita Eid ul-Adh'ha. Katika Idi hii, Waislamu huchinja kwa shauku na jazba kubwa, mbuzi, kondoo, ng'ombe na ngamia kwa idadi ya maelfu na mamilioni. Katika hafla ya Haji, mamilioni ya wanyama huchinjwa huko Makka yenyewe, ambayo ni ngumu kudhibiti. Kisha tunashuhudia pia kwamba watu wanajaribu kujionyesha katika maeneo Fulani na kununua wanyama wakubwa na wa gharama zaidi na kuonyesha fahari katika mazingira yao kwamba tumejitolea sana.




Nchini Pakistani, wameanza kujivunia kwamba hatukuruhusu Waahmadiyya watoe dhabihu ya siku ya Eid al-Adha kwa sababu wao si Waislamu.yaani Wahmadiyya si Waislamu kwa mtazamo wa hawa wanaojiita Waislamu ni Muislamu pekee ndiye mwenye haki ya kuchinja na Waahmadiyya hawezi kuchinja mnyama yeyote. Inashangaza kwamba maafisa wa serikali na vyombo vya haki na kutekeleza sheria vinawazuia Waahmadiyya kutoa dhabihu kwa sababu ya maneno ya hawa wanaojiita wanazuoni wenye maslahi binafsi. Hata hivyo, pale wanapokuwa na baadhi ya maafisa wema, wanawaruhusu Waahmadiyya watoe dhabihu hiyo kwa siri kwa sababu vinginevyo hisia za wanaojiita Maulamaa zinaumia na hali ya fitna na ufisadi inaweza kutokea. Sababu ya wao kufanya

UK. 04

# Mjue Jinni

## Sehemu ya Kwanza.

## Jinni ni nikiumbe gani.?

Jini ni jina la Kiswahili lililotokana na neno la Kiarabu الجن ,al-jinn. Majini ni viumbe wanaosadikika kuishi katika mazingira ya kila aina jambo hili ni sahihi kama tutakapo eleza kwa undani hapo baadae, lakinza tuna angazia mtazamo wa watu wengi ambao bado hawaja ufanyia utafiti wa kutosha au unaweza kusema udhaifu wa kuto kuwa na elimu. **watu wengi wanaamini majini ni viumbe wenye uwezo mkubwa wa kufanya vitu tofautitofauti, pia ni wenye uwezo wa kujibadilisha katika hali ya maumbile kutoka moja kwenda jingine.** Asili ya imani hiyo haijajulikana vizuri ilianzia wapi, lakini ilikuwepo Uarabuni kabla ya Mtume Muhammad [s.a.w]. Kwa asilimia kubwa wenye imani ya uwepo wa majini wanasema ni viumbe wasioweza kuonekana na wenye uwezo wa kumuathiri mwanadamu, Pia ni vigumu kupata uthibitisho wa wazi au wa moja kwa moja kuhusiana na viumbe hawa. Kadiri ilivyo imani hii ya majini ina aminika kuwa waliumbwa na Mwenyezi Mungu kwa kutumia moto na wakiwa wa jinsia mbili tofauti, walikuwepo tangu kuumbwa kwa Adamu a.s mpaka alipokuja Mtume Muhamad[saw] pia walikuwepo. Lakini tunapata mshangao kuwa kama imani hii ya majini

UK. 3

# HEKIMA YA DHABIHU

***Asemavyo Masihi aliyeahidiwa[as]***

Anasema Hazrat Masihi Aliyeahidiwa[as]: "Allah Ameeleza mifano katika sheria ya kiislamu kwa ajili ya maamrisho muhimu. Kwa mfano, mwanadamu ameamrishwa ajitolee katika njia ya Allah kwa nguvu zake zote na mwili wake wote. Basi dhabihu za kidhahiri zimefanywa kuwa mfano kwa hali hiyo. Lakini shabaha hasa ndiyo dhabihu anayoeleza Allah

لن ينال الله لحومها ولا دماؤها ولكن يناله التقوى منكم

yaani nyama za dhabihu zenu hazimfikii Mungu wala damu yao lakini unamfikia utawa wenu- yaani mcheni mpaka mkajifie katika njia yake na jinsi mnavyochinja dhabihu kwa mikono yenu kadhalika mjitolee katika njia yake"

***(Chashma'e Ma'arifat, Uk. 99)***

UTAKASO WA NYOYO

"Utakaso wa nyoyo ndio dhabihu ya kweli, nyama na damu sio dhabihu ya kweli. Watu wa kawaida huchinja wanyama lakini watu maalumu huchinja nyoyo zao. Allah Hakuzuia dhabihu hizi pia ili ijulikane kuwa dhabihu hizo pia zinamhusu mtu."

***(Barahin-i- Ahmadiyya, juz. 5)***

**UBORA WA MAFUNDISHO YA UISLAMU**

"Mimi nadhamba dhabihu hizi katika sheria yetu ng'avu hazihesabiki, na

UK. 08

MZEE SAIDI BAKARI SASAMKA KWA ALLAH KAREJEA >UK .09

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

# SOMO KUTOKA GHANA

Wakati ndugu zetu wa Ghana wanaadhimisha karne moja toka Jumuia ya Ahmadiyya iingie nchini mwao kwa kupitia kazi nzuri iliyotukuka ya Sahaba m.aarufu wa Masihi alieahidiwa Maulvi Maulana Abdul Rahman Nayyar[ra], mambo mawili yamejitokeza kwa shani kubwa na nikielelezo kisicho na shaka cha mafanikio yao. Toka mwanzo hata kabla Sahaba wa Masihi alieahidiwa[as] hajakanyaga ardhi hiyo ya Ghana waghana walikwisha tambua umuhimu, faida na baraka ya kumuandikia Khalifatul Masih[atba]. Ndio wao waliomuomba awatumie Mubashir. Nae akawapa maelekezo ya kuchangishana nauli ya Mubashir kwenda Ghana nao wakafanya hivyo kwa mapenzi, jazba kubwa. Toka wakati huo Ghana haijawahi kutizama nyuma. Waghana wamejijengea utamaduni mkubwa wa kumuandikia mara kwa mara Huzur. Wakulima, wafanyakazi, wanafunzi kwa kuwataja wachache hawafanyi chochote mpaka wamtaarifu Huzur kwa kumuomba ushauri na maombi yake. Maisha ya Mghana kwa ujumla yamezunguka baina ya yeye na Huzur. Jambo la kwanza Mghana analofanya akipata mtoto ni kumuandikia Huzur ampatie Jina. Huu ni utamaduni ambao tunatakiwa Kuiga, na tumeruhusiwa na Quran ***Tukufu fastabikulkhairaat.*** Kila mwenye fikra kwamba Huzur ana shughuli nyingi na hivyo hana muda wa kusoma barua yake hamtendei haki Huzur. Mara kwa mara Huzur amesema kwa msaada wa Allah ana muda wa kutosha kuwatumikia Binaadamu. Tutumie fursa hiyo adimu na adhimu. Hata hivi karibuni Tanzania ilipata uge kutembelewa na katibu wa Huzur anaeshughulika na Answarullah

Ujumbe wake kwa siku mbili za semina ya kimataifa ya Answarullah na baadae ni wito alioutoa kwa wanajamaat kumuandikia Huzur jambo lolote linalowasibu. Faida kubwa imepatikana na ushuhuda mwingi umewekwa bayana na wale ambao wamefaidika kwa kumuandikia Huzur. Jambo jingine la muhimu na la kuzingatia ni kufuata maelekezo ya Huzur. Tazama Waghana kwa haraka walivyochanga pesa na kuzituma Qadian kwa ajili ya Mubashir kuja Ghana. Kuitikia bila kupoteza muda maagizo yote ya Huzur ndio siri kubwa ya mafanikio. Wale unaowasikia wakisifia kazi nzuri inayofanywa na Jumuia Duniani walitakiwa waelewe ya kwamba chimbuko lake ni sisi kufungamana na ukhalifa. Nje ya ukhalifa kuna mahangaiko na majuto. Tujifunze nasi kusikiliza kauli inayotolewa na Huzur na kufanya haraka kutekeleza maagizo yake. Maagizo hayo yanakuja kwa njia nyingi ikiwemo kusikiliza hotuba za Ijumaa za Huzur kuangalia MTA na miongozo wanayopewa viongozi wetu. Nasi pia Insha-Allah tuna miaka michache kabla hatujafikisha karne moja toka Ahmadiyya kuingia Tanzania 1934 Mwaka 2034 akipenda Allah tutafikisha karne kwa Ahmadiyya kua nchini. Tumepata bahati ya kujifunza kutoka kwa ndugu zetu wa Ghana. Hekima kama alivyosema Mtume[saw] ni mali iliyopotea ya mwaminio popote unapoikuta ichukue. Sisi tuna Bahati kuiokota hekima kutoka kwa ndugu zetu. Hekima hiyo ni kujenga utamaduni wa kumuandikia Huzur mara kwa mara na kutekeleza kwa jazba na shauku kubwa maagizo kutoka kwake.



# QUR'AN TUKUFU

قَدْ صَدَّقْتَ الرُّؤْيَا ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ.
. إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ الْبَلَاءُ الْمُبِينُ
وَفَدَيْنَاهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ .
وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْآخِرِينَ

Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyo Tuwalipavyo watendao mema.
Bila shaka (jambo) hili ni jaribio la bayana. Na Tukamkomboa kwa dhabihu kubwa. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye.



# NUKUU YA HADITHI

إني عند الله في أم الكتاب لخاتم النبيين وإن آدم لمنجدل في طينته، وسأنبئكم بتأويل ذلك: دعوة أبي إبراهيم، وبشارة عيسى قومه، ورؤيا أمي التي رأت أنه خرج منها نور أضاءت له قصور الشام،.
(المحدث: شعيب الأرناؤوط في تخريج المسند لشعيب – ١٧١٦٣ الراوي: العرباض بن سارية )

Tafsiri: kwa Yakini mimi ni Khatam un nabiyyin mbele ya Allah Mtukufu katika ummu ul Kitab ilhali Adam alikuwa baado kuchanganywa udongo wake, nami nitawaelezeni ukweli wake. Mimi ni mwito wa babangu Ibrahim. Na bishara ya Issa kwa watu wake. Na ndoto ya mama yangu, aliyoiona kwamba Nuru imetoka kwake na ngome za Syria zilinga'a kwayo.

## Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Kwa hakika kulikuwa na siri kubwa ndani ya siku hiyo kwamba, dhabihu , aliyoipanda mbegu yake Ibrahim a.s. kwa siri, Mtume s.a.w. alionyesha mazao yake ya kudumu. Hazrat Ibrahim a.s.hakusita katika kumchinjia mwanaye kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Kulikuwa na somo ndani yake kwa siri kwamba mtu awe wa Mungu kwa pande zote na mbele ya amri ya Mungu, uzima wake, kizazi chake,ndugu zake na damu ya wapenzi wake, ionekane hafifu. Katika enzi za Mtume s.a.w.,aliyekuwa mfano kamili wa kila mwongozo uliotukuka, dhabihu ya namna gani ilitolewa? Pori zimejaa na damu kana kwamba mito ilitiririka na damu. Wazazi waliwaua Watoto wao, na Watoto waliwaua wazazi nao walikuwa wanafurahi kwamba kama wanasagwa katika njia ya Mwenyezi Mungu na kukatwa vipand vipande basi itakuwa raha kwao."
(Malfoozat.J.1.u.k.327 chapa ya 1988)

## MANENO YA SEYDNA AHMAD[AS] JUU YA QUR AN TUKUFU

Kurani Tukufu ndicho kitabu chenye fahari kuu kiasi hiki kwamba hapana kitabu kingine kinachoweza kuipita katika fahari yake.

Ndicho Al-Hakam, kikiwa kitabu ambacho uamuzi wake ndio wa mwisho; ndicho Muhaiman, yaani: Ni muhtasari mzima wa kila mwongozo. Ndani yake yapatikana kila hoja mtu awezayo kuhitaji.

Ni kitabu hiki ambacho kimeitimua kwa ushindi nguvu ya maadui. Kitabu kinachozungumzia kila kitu kwa undani na kinazo habari za yale yaliyokuwepo na yale yatakayo kuwepo.

Batili haiwezi kukishambulia toka mbele wala nyuma. Ndicho nuru halisi ya Mungu Mweza.

(Roohani Khazain Jal. ١٦, Uk. ١٠٣: Khutba Ilhamiya Uk. ١٠٣).

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

# Mjue Jinni

*Kutoka 1..*

ilikuwepo kabla ya ujaji wa Mtume s.a.w kwanini waislam wana shikilia imani hii kwa nguvu sana tena kwa kuwaaminisha watu kuwa yana uwezo wa kuwapanda vichwani na hasa wanawake na kuwafanya wakristo waamini Islam ni dini ya majini.

Wakristo husema kuwa Wislamu huamini kuna majini wazuri na majini wabaya kwa maana ya madhara yao katika maisha ya mwanadamu na badhi ya Waislamu (pengine wasiofuata misingi sahihi ya Uislamu wao) hufuga majini hao katika nyumba zao au miili yao na wengine kuaminisha watu kuwa wana uwezo wa kuwatupia majini au kuyaondoa.

Pia huwafanya viumbe hao kama wasaidizi au walinzi wa maisha yao kwa wale ambao huamini ni majini wazuri. Lakini wengine hutumia pia majini waitwao wabaya kuharibu na kutesa maisha ya watu wengine kwa kuwatuma kuwaingia miilini na kuleta magonjwa, kuharibu kazi au biashara ya mtu na hata familia. Ingawa wapo wanaoamini uwezekano wa majini kutengenezwa na watu, imani inakanusha hili. **"Sema: Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa kila kitu na yeye ni mmoja mwenye kushinda" (Raad 13:17).** Isipokuwa Waislamu wanaamini uwezekano na kuwatumia maji namna mbalimbali. Katika aya hii tunapata kujua hakuna anaye weza kuumba majini, labda majini wakufikirika ndiyo wanaweza kuumba ambao nao hawata dumu.

Pengine ulishawahi kukutana na mtu au watu wakikueleza juu uwepo wa majini wazuri, na wabaya wakakueleza jinsi wanavyo weza kuyatoa. Pia huwa wana wataja kwa majina kwa mfano Jini subiani, Jini Maimuna, Jini Makata, Jini Ruhani, Jini mahaba, Jini bahari na haya ni majina machache kati ya mengi ambayo huwa wana ya eleza ama kutaja.

Habari hizi zinazo husiana na majini zinazidi kutapakaa kwa watu kadri siku zinavyozidi kwenda. Nawengi humfahamu Jini ni kiumbe cha ajabu ambacho hakioneka macho na hufanya watu kukiogopa zaidi. Na kiumbe hiki kina uwezo wa kuingia katika mwili wa binadamu, na mtu kuwa na uwezo wa kuweza kufanya kitu kilicho nje ya uwezo wake wa kawaida.

**Huo ulikuwa mtazamo wa watu na jinsi gani wanavyo chukulia uwepo wa jinni. Sasa tunaelekea kwenye kujua ukweli wenyewe hasa juu ya Majini.**

Tukisoma Quran jini huyu ametajwa katika Qur-an Tukufu katika sehemu mbali mbali, Na ndio maana wanasema huu ni uthibitisho tosha wa uwepo wa Jini ulimwenguni na wanao weza kumiliki majini hao ni waislam na watu wenye dhambi tu. Hivyo basi nataka tufahamishane kuwa ni Jini gani aliyetajwa katika Qur-an tukufu ili tuweze kuepukana na msiba mkubwa huu wa kumshirikisha Mwenyezi Mungu na kutumia vibaya aya za Quran kwa kuwaaminisha watu Majini wenye kupanda vichwani mwa wanawake.

Aya hii ifuatayo ndiyo inayochukuliwa kuwa ni kitambulisho cha uwepo wa Jini ulimwenguni.

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

Na sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. **[51:57]**

Hapa ndipo watu wengi wanadai kua Mungu ameumba Jini ambae ni kiumbe wa ajabu, kwa kwamtazamo wa haraka kweli utaona hapa Jini ametajwa na mwana damu. Lakini hapa pana hitaji kufasiriwa ili kupata falsafa yake hasa na ni nikiumbe gani huyo anaefahamika kuwa ni kiumbe wa ajabu mwenye jina la jini. Kwanza kabisa neno (جِنَّ) ni neno la kiarabu na neno hili katika kamusi za lugha ya kiarabu lina maana ya **kufunika** kwa **maana ya kitu kisicho onekana kwa macho**, neno (جِنَّ) limetumika pia katika sura Al-anaam katika aya isemayo;

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ اللَّيْلُ رَأَىٰ كَوْكَبًا ۖ قَالَ هَٰذَا رَبِّي ۖ فَلَمَّا أَفَلَ قَالَ لَا أُحِبُّ الْآفِلِينَ

Na ulipo mfunika usiku akiona nyota, akasema: Huyu ni Mola Mlezi wangu. Ilipo tua akasema: Siwapendi wanao tua. [6:77]

Hapa limetumika neno (جَنَّ) ambalo mzizi wake ni hilohilo jinni, kama neno hili (جَنَّ) tukilipa maana ya kiumbe cha ajabu neno hilo lingalileta maana ga Ibrahim au na mwezi haujawahi pia kuonekana kwenye macho ya watu na unaonekana kwa siri tu tena na watu wachache? Kama ingalikua neno جِنَّ linapotajwa linamaanisha kiumbe wa ajabu basi na hapa lisingelikuwa na maana nyingine iwayo ispokuwa hiyo hiyo ya kiumbe wa ajabu. Kwa ujumla naweza kusema kwamba hakuna uthibitisho wa wazi wa kuwepo kiumbe hicho cha ajabu kinachoitwa Jinni.

Ikumbukwe ya kwamba neno جِنَّ linapo tumika mahala Fulani katika Quran basi hakuna kiumbe kingine zaidi ya binadamu anaye elezwa hapo.Tukumbuke ya kwamba Qur-an haikuteremshwa kwa ajili ya kiumbe kingine chochote duniani ispokua mwanadamu na kuamriwa atekeleze hukumu zote za Quran na sio jini. Kama anayvosema Allah katika ayah ii:

إِنَّا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ بِالْحَقِّ ۖ فَمَنِ اهْتَدَىٰ فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَمَا أَنْتَ عَلَيْهِمْ بِوَكِيلٍ

Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu kwa ajili ya watu wote kwa Haki. Basi mwenye kuongoka nafsi yake, na mwenye kupotoka bila ya shaka amepotoka kwa hasara ya nafsi yake. Na wewe si mlinzi juu yao. **[39:42]**

أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ لِلنَّاسِ

...tumekuteremshia kitabu kwa ajili ya watu....

Tunajua vizuri ya kwamba Qur-an ni kitabu alichoteremshiwa Mtume Muhammad[saw], ili kiwe ni mwongozo na rehma kwa walimwengu, na pia kiwaonye. Na tunapo wazungumzia walimwengu hatumaanishi kua ni viumbe wengine tofauti na binadamu. Kama Qur-an imeshushwa kwa ajili ya watu basi haiwezi kumnufaisha mnyama wala ndenge wala kiumbe kingine chochote kile kinyume na mwanadamu. Kuna watu wanasema kuwa viumbe hawa yaani majini wamepata kuisikia Qur-an Tukufu ikisomwa na wao wakasilimu wakawa waislam.

Na aya yenyewe ni hii;

قُلْ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ اسْتَمَعَ نَفَرٌ مِنَ الْجِنِّ فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا

Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur´ani ya ajabu.[71:2]

يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ ۖ وَلَنْ نُشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا

Inaongoza kwenye uwongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi. [71:3]

وَأَنَّهُ تَعَالَىٰ جَدُّ رَبِّنَا مَا اتَّخَذَ صَاحِبَةً وَلَا وَلَدًا

Na kwa hakika utukufu wa Mola wetu Mlezi umetukuka kabisa; hana mke wala mwana.

وَأَنَّهُ كَانَ يَقُولُ سَفِيهُنَا عَلَى اللَّهِ شَطَطًا

Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikuwa wakisema uwongo ulio pindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu. [71:5]

Hizi ni baadhi ya aya za suratul jinni, na ndio sura inayo pewa kipaumbele kuwa imewataja hao viumbe wa ajabu wanao itwa majini. Je nikweli majini yaliyotajwa hapa ni viumbe hivyo wanavyo vidhania wao?

Hapa majini wanasema wameisikia Qur-an ya ajabu. Inayoongoza katika uongofu, kwa hivyo tumeiamini.

Na kwa hakika utukufu wa Mola wetu umetukuka kabisa na hana mke wala mwana. Na kwa hakika wapumbavu miongoni mwetu walikua wakisema uwongo uliyo pindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu. Kwenye maneno haya tunapata kuona ya kuwa kundi moja la majini limesilimu, pia wakaamini kuwa Allah hana mke wala mtoto, na pia wanasema wapumbavu miongoni mwao walikua wakisema uwongo ulio pindukia mipaka juu ya Mwenyezi Mungu, upumbavu upi huo ndiyo huu tu kusema Mwenyezi Mungu hana mtoto na kiuhalisia tunaona leo wanao sema Mungu ana mtoto ni akinanani je bado tunahitaji kujua jinni ni nani na jinni mwenyewe ndio mapadre na serikali zao walio tumia nguvu kuhubiri kuwa Mungu ana mwana na Mayahudi pia wana madai kama hayo kuwa Mungu ana mtoto.

Kama anavyosema Allah katika ayah ii kuwa.

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَٰنُ وَلَدًا

Na wao husema kuwa Arrahmani Mwingi wa Rehema ana mwana![19:89]

UK. 04

# Mjue Jinni

*Kutoka Uk 01..*

تَكَادُ السَّمَاوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا

Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. [19:91].

أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَٰنِ وَلَدًا

Kwa kudai kwao kuwa Arrahmani Mwingi wa Rehema ana mwana.[19:92]

Hizi ni aya za Suratul Maryam ambazo Mungu anawakanusha wale wanaodai kuwa Mungu ana mtoto, Hapo majini wanakiri kuwa wapumbavu miongoni mwao wamemzuilia Allah uwongo, na uwongo wanaomzulia Allah ni kudai kuwa Mungu ana mtoto pia hatomleta tena Nabii, katika Sura hiyo hiyo majinni wanasema.

وَأَنَّهُمْ ظَنُّوا كَمَا ظَنَنْتُمْ أَنْ لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ أَحَدًا

Na kwa hakika wao walidhani, kama mlivyo dhani nyinyi, ya kuwa Mwenyezi Mungu hatamleta Mtume. [72:8]

Sawa na maelezo ya aya majini wanasutana wenyewe kwa kusema kuwa walidhani kama mlivyo dhani ninyi kua Mungu hatomleta tena nabii, nahii inaonyesha ni kawaida ya watu sio majini maana kauli kama hii inapatikana kwenye **sura Almumin 40 aya ya 35 Nabila shaka zamani aliwafikieni Yusuf kwa dalili zilizo wazi, lakini ninyi mkaendelea na shaka kwa yale aliyo waleteeni: mpaka alipo fariki mkasema, Allah hataleta kabisa Mtume baada yake**, hawa watu ambao imani zao ni dhaifu na wanamkadiria Mwenyezi Mungu uwezo wake au amri yake ya kutuma mitume Duniani. Ndipo Mungu anaonesha uwezo wake kwa kumleta Nabii mwingine kuweza kukanusha zile dhana zao kuwa Mwenyezimungu hato leta mtume.

Sasa kwa mujibu wa Suratul Jinni inaeleza watu wanao mfanya mtu kuwa Mungu ni wenye makosa. Basi tupewe ushahidi wa kuwa imani za watu zipo sawa na za hao majini na je Mungu alileta mitume wangapi kwa majini na Majini hayo yenye kuamini Mungu ana mwana ni majini yapi na pia tupewe ushahidi wa Mtume wao alikua ni nani?

Ijulikane kwa uwazi kabisa mitume wote walio letwa na Mwenyezi Mungu walikua ni wanadamu kama sisi na waliletwa kuongoza kwenye tauhiidi ya Mungu mmoja. Na ni jambo lililo la kweli kabisa kwani majini waliyotajwa kwenye Quran ni Wkristo na Mayahudi wenye mamlaka katika nchi au ufalme ndio wanao shika imani ya Mungu kuwa na mtoto. Na wale walio sikia Quran ni wale wenye vyeo vidogo vidogo na wakajua ukweli juu ya imani ya umoja wa Mwenyezimungu. Katika historia na Hadithi vinaonyesha hawa majini walikuwa ni binadamu toka kwenye imani ya ukristo na waliomba kukutana na Mtume Muhammad[saw] katika muda Fulani wa usiku ili wao wasijulikane kuwa walienda kumuuliza nini Muhammad s.a.w na wakawa wenye hatia lakini Allah aliweka wazi katika sura jinni mazungumzo yao baada ya kutoka kwenye kikao kile ili kutufahamisha kuwa wale walikuwa ni watu. Kwahakika Qurani ilikuja kuongoza watu na wengine wana tabia kama za watu waliyo pita, na Allah anaeleza tabia hoyo kwenye aya ifuatayo.

وَلَقَدْ جَاءَكُمْ يُوسُفُ مِنْ قَبْلُ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا زِلْتُمْ فِي شَكٍّ مِمَّا جَاءَكُمْ بِهِ ۖ حَتَّىٰ إِذَا هَلَكَ قُلْتُمْ لَنْ يَبْعَثَ اللَّهُ مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا ۚ كَذَٰلِكَ يُضِلُّ اللَّهُ مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ مُرْتَابٌ

Na alikwisha wajieni Yusuf zama dalili zilizo wazi, lakini nyinyi mliendelea katika shaka kwa yale aliyo kuleteeni; mpaka alipo kufa mkasema: Mwenyezi Mungu hataleta kabisa Mtume baada yake. Kama hivyo Mwenyezi Mungu humwacha kupotea anaye pindukia mipaka katika maasi anaye jitia shaka. [40:35]

Je hapa napo ni majini hawa wenye Imani ya kusema Mungu hatamleta nabii mwingine? Kiukweli suratu jinni haiwazungumzii majini hao wanao wafahamika kwenye Jamii kuwa ni viumbe wa ajabu, bali inawazungumzia watu kama sisi ambao baadhi yetu ni watu wa kawaida na wengine ni viongozi wenye mamlaka fulani katika nchi.

Soma na habari hii pia inayo patikana kwenye aya hii isemayo:

يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِنْكُمْ يَقُصُّونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِي وَيُنْذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا ۚ قَالُوا شَهِدْنَا عَلَىٰ أَنْفُسِنَا وَغَرَّتْهُمُ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا وَشَهِدُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ أَنَّهُمْ كَانُوا كَافِرِينَ

Enyi makundi ya majini na watu! Je, hawakukujieni Mitume kutokana na nyinyi wenyewe wakikubainishieni Aya zangu, na wakikuonyeni mkutano wa Siku yenu hii. Nao watasema: Tumeshuhudia juu ya nafsi zetu. Na yaliwadanganya maisha ya dunia. Nao watajishuhudia wenyewe ya kwamba walikuwa makafiri. [6:131] na [55:34]

Hapa wanaambiwa majini na watu je hawakufikieni mitume kutoka miongoni mwenu ninyi wenyewe wakikubainishieni aya Zangu? kwa mujibu wa aya hii hata majini nao wameletewa Mtume anaetokana na wao, sasa ilikuaje wakaacha kitabu chao na kufuata Quran ambacho si kitabu chao? Binadamu pia hatuwezi kufata kitabu cha majini kuwa mwongozo wetu ilhali tuna Nabii wetu.

mba hakuna kiumbe kama huyo aliye jificha aitwaye Jini na kiumbe anaye zungumziwa ni binadamu tu. Kama haitoshi tusome na aya hii:-

وَلِسُلَيْمَانَ الرِّيحَ غُدُوُّهَا شَهْرٌ وَرَوَاحُهَا شَهْرٌ ۖ وَأَسَلْنَا لَهُ عَيْنَ الْقِطْرِ ۖ وَمِنَ الْجِنِّ مَنْ يَعْمَلُ بَيْنَ يَدَيْهِ بِإِذْنِ رَبِّهِ ۖ وَمَنْ يَزِغْ مِنْهُمْ عَنْ أَمْرِنَا نُذِقْهُ مِنْ عَذَابِ السَّعِيرِ

Na Suleiman tuliufanya upepo umtumikie. Safari yake ya asubuhi ni mwendo wa mwezi mmoja, na safari yake ya jioni ni mwendo wa mwezi mmoja. Na tukamyayushia chemchem ya shaba. Na katika majini walikuwako walio kuwa wakifanya kazi mbele yake kwa idhini ya Mola wake Mlezi. Na kila anaye jitenga na amri yetu katika wao, tunamwonjesha adhabu ya Moto unao waka. [34:13]

***Mola wetu tupatie elimu ya kutosha kuhusu Jini na uwezo wa kuwaelewesha watu ambao kwa sasa wamevuka mipaka katika kumwelewa jinni na kufanya Jamii iuchukulie uislam kuwa ni dini mbaya. Utufanye tuwe wenye kufuata miongozo na mafundisho ya manabii na makhalifa wako ili tusivuke mipaka kama wengine. Amiin.***

# Kuzingatia Ucha-Mungu kwenye kila kitendo n i j u k u m u l e t u .

*Kutoka Uk 01..*

hivi sababu watu hawa hawana uchamungu. Wanadhamba kwa kufanya makosa hayo kwa jina la Uislamu, kwa jina la Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (SAW) Kufikia viwango vya juu vya utumishi na wema. Siku moja Mungu ataamua ni watu gani wanaotembea katika uchamungu. Vigezo vya wema ni vipi? Ni nani aliye sahihi na ni nani asiyefaa machoni pa Mungu Mwenyezi? Ikiwa tutaendelea kumuelekea Allah Taala huku tukitembea juu ya Taqwa, basi hakika nusura ya Allah Taala itakuwa pamoja nasi, Mwenyeezi Mungu akipenda.

Katika Surah Hajj, Mwenyezi Mungu Amesema kwamba ikiwa hakuna uchamungu,basi Mwenyezi Mungu hatakubali dhabihu zenu za wanyama wakubwa wakubwa na wa gharama kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu hahitaji nyama na damu zenu. Yeye Ametakasika na mahitaji haya. Kwa hiyo hatuna haja ya kuwa na wasiwasi kwamba tulizuiwa kutoa dhabihu, au kwamba viongozi wa dini au maafisa wa serikali walitunyang'anya wanyama wetu, au kwamba nyama ya wanyama waliochinjwa ilichukuliwa. Allah Ta'ala Anasema kwamba ikiwa tutakusudia kutoa dhabihu hii huku tukifuata Taqwa na kuitekeleza ni maqul kwangu(itapokelewa nami) na ikiwa ni dhabihu isiyo na uchamungu, basi ni kuchinja tu mnyama bure isiyofaa kabisa. Kwa hiyo, ni kazi yetu kuzingatia uchamungu katika kila tendo letu.

[Al-Fazal International ya tar.23 Julai 2021]

# Ukhalifa, Uongozi bora na uliotukuka

*...Kutoka tolro lililopita*

**Na. Sheikh Karim-ddin Shamsi Sahib**
**Morogoro**

**Khalifa wa nne** wa Seyyedna Ahmad[as] aliwahi kutuelezea hali yake kwa maneno haya kwamba: "Baadhi ya usiku ninakesha na kumlilia Mungu juu ya shida na taabu za wanajamati."

Safari moja, **Khalifa wetu wa tano** alisema akieleza hali yake halisi kwamba:"Khalifa wa zama anakuwa na uhusiano wa dhati na kila muahmadiyya wa kila taifa, na wa kila kabila, wa dunia nzima. Anapata barua zao za dhati kabisa zielezayo mambo yao ya dhati, huu ndio ukhalifa tu unaojali shida ya kila Muahmadiyya wa duniani. Khalifa anawaombea dua. Ni nani miongoni mwa viongozi wa dunia hii ambaye huwambea wagonjwa. Ni nani anayesikitika juu ya mambo ya ndoa ya wasichana wa taifa lake na kuwaombea dua, …… Wanajamati ndio wenye bahati nzuri ambao huwaombea dua khalifa wao, anasikitika kwa ajili ya afya yao, elimu yao, na mambo yao ya ndoa, kwa kifupi, hakuna tatizo lolote la waahmadiyya wa duniani ila khalifa analijua na kujitahidi kwa ajili ya kuliondoa na kuwaombea dua. Mimi pamoja na makhalifa waliokuwa kabla yangu pia walikuwa wanafanya hivyo, mimi nimejaribu kueleza kidogo kutoka katika shuguli nyingi za khalifa alizopewa na Mungu na anapaswa kuzitekeleza. hakuna nchi duniani ila nafika huku kwa mawazo yangu kabla ya kulala na kuwaombea dua hata wakati ninapoamka pia nawaombea dua.

Ukhalifa wa kiahmadiyya tu unaoweza kuleta mabadiliko na mapinduzi ya kweli, Hadhrat Musleh Maud[ra]. alisema, kumbukeni ya kuwa maendeleo yenu yote yamo katika kujiunga na ukhalifa na siku ambapo mkisahau jambo hili na kughafilika nalo basi siku hiyo itakuwa siku yenu ya mwisho, lakini endapo mtaendelea kushikamana na Ukhalifa basi lau kama Dunia nzima itaamua kuwaangamizeni haitaweza kufanya cho chote.

Huzur anasema; ''Mtu yule tu anaweza kufanya kazi ya silsila hii ambaye anajiunganisha na Imamu. Na kama mtu yoyote hajiunganishi na Imamu ingawa anajua elimu yote ya dunia hawezi kufanya kazi ya silsila.

Siku moja hazrat Chauhdary Muhammad Zafrullah Khan alipoulizwa kuhusu mafanikio yake alijibu bila kutafakari kwamba: nilikuwa mtiifu kwa khalifa siku zote.

Maneno haya ni ya kweli kabisa. Wakati Fulani Hazrat Sir Zafrullah Khan sahib aligombea nafasi ya Mbunge huko Sialkot na alikuwa na Yakini kamili kwamba atashinda basi mgombea mwenzake Sir Shahab alifika kwa khalifa wa pili na kumuomba kwamba amzuie Chauhdary Sahib asigombee safari hii na ajitoe kwenye uchaguzi kisha atagombea safari nyingine. Huzur khalifa wa pili alikubali ombi la Sir Shahab ambaye hakuwa mwanajamaati na kumpelekea ujumbe Chauhdary Sahib kwa ajili ya kutokugombea basi Chauhdary Sahib alikubali mara moja bila kusita hata kidogo.

Safari moja Hazrat Khalifatul Masih wa pili alisema: kama kujiua isingekuwa marufuku basi ningeweza kuwaonesha watu kwamba kama nawaamuru watu 100 miongoni mwa wafuasi wangu ili wajiue mara moja basi wao wangefanya tu na dunia ingeweza kushuhudia tukio la uaminifu wao mkubwa kwa ukhalifa.

Khalifa tul Masih wa tatu alipoenda kuzuru ulaya mara ya kwanza basi alikosa kupanda kwenye ndege na kuchelewa kufika hivyo alimpigia simu Chauhdary Zafrullah Khan sahib lakini huzur alihuzunika akisikia sauti yake dhaifu mno na kuhisi kama yeye anaumwa sana. Huzur alimuelezea katibu wake basi Chauhdary Sahib aliitwa kuja kwa huzur lakin alipofika alikuwa mzima wa afya hivyo aliulizwa na katibu mkuu wa Khalifa kuwa amekuaje alipopigiwa simu na Huzur alionekana kama anaumwa sana na kushindwa kuongea basi alieleza kwamba kwa kuwa yeye aliweza kuongea na khalifa baada ya muda mrefu hivyo hakuweza kujizuia hisia zake za upendo uliozidi mno kwa khalifa na alishindwa kuongea na macho yake yalianza kutiririsha machozi.

Sahaba moja wa mtume saw aitwaye Hazrat Saad Alaswad alikuwa mweusi na hivyo alikuwa hapati mchumba akaja kwa Mtume[saw] kumwomba msaada wake. Mtume saw alimtuma kwa Hazrat Amr bin Wahab wa ukoo wa banu Thaqiif bwana huyu alikuwa mwiislamu mpya na alikuwa na binti. Bwana yule alipofika kwa Amr bin Wahab, naye hakumuamini na alikataa kukubali kumuozesha binti yake lakini binti yule alikuwa anasikia yote hivyo alijitokeza na kutoa hotuba nzito akieleza uaminifu na utii kwa Mtume[saw] na kusoma aya ya Kurani kuwa:

**ما كان لمومن ولامومنة اذا قضى الله و رسوله امرا ان يكون لهم الخيرة من امرهم ومَنْ يَّعصِ اللهَ و رسوله فقد ضل ضلالامبينا. الاحزاب:٣٧**

Yaani haiwi kwa muumini mwanaume wala muumini mwanamke, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapoamua jambo,kuwa na hiyari katika jambo lao,na yeyote atakaye muasi Allah na Mtume Wake basi amepotea upotevu ulio wazi.

khalifa wetu mpendwa anasema: "Ushindi wa Islam utapatikana leo kumptia Seyyedna Ahmad[as]. bendera ya mtume mtukufu itapeperushwa na wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa[as], ambao huamini juu ya Ukhalifa, ambao wameshikamana na Ukhalifa, ambao wameshajiunga na Jamaati yake na kushikamana na Kamba ya Allah."insha Allah, huzur anasema akieleza zaidi kwamba,

Zama hizi ni za maendeleo na za ushindi wa Jamaat, naweza kusema kwa yakini kamili kwamba milango ya msaada na nusra ya kiungu imekwishafunguliwa na inaendelea kufunguka kila siku kwa kiasi hiki kwamba maendeleo na ushindi unasogea karibu zaidi kila siku, nasema kwa uhakika na busara zangu kuwa Allah[sw]. Ataendela kutoa msaada wake usiohisabika kwa ajili ya ushindi wetu na hakuna anayeweza kuyazuia maendeleo ya Jamaati.

Mwana historia mmoja ambaye ni mkiristo aliandika:

"Wakiristo kama wanaweza kukumbuka jambo hili litakuwa bora kwao kwamba mafundisho yake Mtume[saw] yalizalisha jazba ile ya dini ndani ya wafuasi wake ambayo kuitafuta kwa wafuasi wa mwanzo wa Masihi ni kazi bure tu. mayahudi walipomtundika masihi msalabani basi wafuasi wake walimkimbia na kuisahau Imani na dini na kumuacha kiongozi wao kwenye mahangaiko ya mauti na kinyume chake wafuasi wa Muhammad[saw] wakajumuyika kwake wakijihatarisha nafsi zao na kumshindisha juu ya madui zake."

(Siratun Nabii J.1. Shibli Nu'umani uk.139-140)

Wasomaji watukufu: Ahadi ya **انی معک یا مسرور** iko pamoja nasi ila tu, tunatakiwa kutimiza ahadi zetu na wajibu wetu kuwa ewe khaalifa wetu mpendwa tupo tayyari kujitolea nafsi zetu, mali zetu na muda wetu kwa amri yako moja na kutii kila agizo lako, hivyo basi enyi wapendwa wa jumuiyya ya Mungu, sasa ni wakati wa kutekeleza wajibu wetu, tuyahuishe mifano ya wazazi wetu waliotangulia kwa sababu sisi pia tumefunga ahadi kama wao, sikilize jinsi gani na kwa upendo wa namna gani khalifa wetu, mpendwa wetu na mpenzi wa Mungu anatuita kwenye kutimiza ahadi zetu, tunapaswa kufunga nia na azma hii leo, kuwa tutakuwa pamoja kama ukuta uliopigwa risasi kwa ajili ya kutii kila amri yake khalifa, tutafuata kila agizo lake na kusema labbaik labbaik ya imamana, mali zetu, heshima zetu, nafsi zetu na uzima wetu ujitolee kwako, sisi ni wafuasi wako wakweli, uzima wetu na kufa kwetu kutakuwa chini ya amri yako ewe khalifa wetu, tutalishika na kulitenda kila neno litokalo mdomoni mwako na leo hii tunakiri tukiwa tunamshahidisha Mungu kuwa, tutakutii kwa namna hii kwamba hata malaika watiifu wa Mungu watashindwa mbele yetu.

Uzuri ulioje wa beti hiyo:

**مبارک وہ حقیقت جان لی جس نے خلافت کی**
**مبارک وہ قیادت مان لی جس نے خلافت کی**
**مبارک وہ جو پیوستہ خلافت کے شجرسے**
**کہ وہ محفوظ ہر خوف وخطر ہر فتنہ گر سے**

Tafsiri: Mwenye mibaraka ni yule anayefahamu uhakika wa ukhalifa, amebarikiwa yule anayekubali uongozi wa ukhalifa,

Mwenye mibaraka ni yule anayefungamana na mti wa ukhalifa kwani amesalimika na kila hofu, kila hatari na kila fitina.

Ewe Mwenyezi Mungu utuwezeshe kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu na majukumu yete. Ewe Mola wetu utujaalie ufahamu, busara na akili na kutupatia mapenzi ya kweli na ya undani kabisa juu ya ukhalifa, na baraka za ukhalifa ziendelea kutushukia milele. Amin!

# Bustani ya Washairi

**MTI**
Mti wetu masikini, ghafla umeanguka,
Pale ndio barazani, tuyuri kukusanyika,
Mashairi kuyaghani, nyoyo zikaburudika,
MTI wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Ndio hapo maskani, kwa wapenda kuandika,
Palikuwa ni chuoni, wanafunzi wakifika,
Ili wamanye kanuni, nini kinahitajika,
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Ndie manju wa zamani, kote aliheshimika,
Akitoka uwanjani, wote wanaburudika,
Vinapambwa na mizani, mahiri wa kuviweka,
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Alitoa na diwani, ya mashairi shufaka,
yaliyotoka moyoni, tusije kuhadaika,
Dunia ni kituoni, safari hatujafika,
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Kulinda utamaduni, hilo alihangaika,
Itukuke yake shani, lugha yetu ya baraka,
Ikue yake thamani, popote kukubalika,
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Nyuma kaacha madini, hivyo tufanye haraka,
Yale pale Kinondoni, na kwengine kadhalika,
Tukusanye kwa makini, pasi moja kuponyoka
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Yarabbi Mola manani, machozi yatiririka,
Twawaombea imani, wafiwa yalowafika,
Sote tuko safarini, mwenzetu ameshafika
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

Kalamu naweka chini, tutabaki kukumbuka,
Mema yake Duniani, nyumba yetu kuezeka,
Naye apate peponi, dar ilokamilika,
Mti wetu kuanguka, ndege watatua wapi?

***Mahmood Hamsin Mubiru ( Wa Mamba)***
***5:51, 02/05/2024***

**KILIO**
(1)Kichwa tumejinamia , machozi yatumwagika.
Pale tuliposikia, Andanenga katutoka.
Tunakuomba Jalia, mlaze pakutukuka.
Mlaze pakutukuka Amiri wa Andanenga.

(2)Amiri wa Andanenga, kwetu tutamkumbuka,
Mno alitupa mwanga, mahiri wa Kila Rika.
Kwa weledi alitunga, mashairi kusikika.
Mlaze pa kutukuka, Amiri wa Andanenga.

(3) Katuachia mapenzi, Andanenga msifika.
Niwetu wetu kipenzi, taa imesha zimika.
Mashairi Hadi tenzi , huyo gwiji kaandika
Mlaze pa kutukuka, Amiri wa Andanenga.

(4)Mkuzaji kiswahili, sanifu za uhakika.
Pengo ni kubwa kwa kweli, ambalo limetufika.
Tunakuomba Jalali, peponi kumpeleka.
Mlaze pa kutukuka, Amiri wa Andanenga.

(5)Usia Katuachia, Mashairi kuandika
Fani kuipigania, pembeni sije iweka.
Ndilo la kuzingatia, upendo wa itajika.
Mlaze pa kutukuka, Amiri wa Andanenga.

(6)Kalamu naiachia, moyoni nasikitika.
Nguvu zimeniishia, niwapi tutaposhika.
Ametutoka jamia, mlezi asiyechoka.
Mlaze pa kutukuka, Amiri wa Andanenga.

Bi.Moza Juma Mtambo
Mtongani /DSM
Simu 0750 631949

**MSHAIRI ANDANENGA**
Imetuzimika taa, karabai si kandili,
Kwa hakika iling'aa, kwa wake mwanga mkali,
Na kwenye hili jukwaa, iliwaka kwelikweli,
ametuondoka nguli, MSHAIRI ANDANENGA.

Kifo hakina shujaa, awe mkaba kabali,
yeyote kitamvaa, mwenye nguvu kama nduli,
mwingine kwenye rakaa, ibadani akiswali,
ametuondoka nguli,MSHAIRI ANDANENGA.

Pole ndugu na jamaa, na viunga mbali -mbali,
poleni wana sanaa, pole wana kiswahili,
zaramo na usambaa, na wengine tukubali,
ametuondoka nguli,MSHAIRI ANDANENGA.

Mziwanda nanyamaa, si nyingi nilosaili,
makiwani ninakaa, japo nidhoful'-hali,
nabakia na butwaa, katuondoka jabali,
ametuondoka nguli,MSHAIRI ANDANENGA.

Abdallah luhinda mziwanda mwanza.
0757616808.
Adimini muunge huyu ni mshairi nguli sana tupo naye huku Mwanza.
0757443357.

**KIFO CHA ANDANENGA**
Dakika na zake saa zimepita kwenye Anga,
Imenipata fazaa machozi yakinilenga,
Kwa kuzima ile Taa iloikinipa Mwanga,
Rabi amweke Andanenga mahali pema Peponi.

Tunakuomba Manani mweke Pema Andanenga,
Mjao mwenye Imani Dike ndiyo kinga,
Umemwita Rahmani kaitika hakupinga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Andanenga Mhimili wa Tarjumi na Kunga,
Mjuzi wa Kiswahili na Mashairi kutunga,
Mwenye nyingi Taamuli Lugha yetu kuijenga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Si pekee Usanii ulompa Unyakanga,
Ni Galacha na Karii ni mwenye mema kulenga,
Kafanya kila bidii kuzongoa yalozonga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Katupa kubwa Elimu Penseli tukachonga,
Tukajawa Ufahamu kujua Dema na Tenga,
Leo kawa Marehemu papo patapojifunga
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Lugha kaipamba pambo Lugha kaiengaenga,
Palipokuwa na Shombo kuandika na kulonga,
Alifanya kulihali matumizi kuyachunga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Ametufanyia mengi ya watu mbele kusonga,
Mengi sana ya Msingi pasipo kuvungavunga,
Kaviondoa vigingi tangu enzi za Wahenga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Nakushaurini nyote tuyaanue Matanga,
Machozi yetu tufute Dua kwa Mola kupanga,
Pepo ya Mola apate aipate Andanenga,
Rabi mweke Andanenga mahali pema Peponi.

Mshauri Mkuu,
DK. Kassim.M.P Haumotile (Mndewa wa Sungwi)
Mwenyekiti wa Uwashata Taifa.
Simu 0713 340777, 0782 340777
Dsm.

**ANDANENGA KAONDOKA**
Habari zimesikika, za umma kutahayari,
va kwamba imezimika, nuru iliyonawiri,
Hivyo kiza kugubika, katika yote Sayari,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Andanenga kaondoka, kwenye chombo kaabiri,
Dunia ameitoka, ameshafunga safari,
Mwendo umemalizika, na hii ndio habari,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Kwa kweli alizeeka, alishavuka kadiri,
Tisini na minne Myaka, ni huo wake umri,
Mwili ulikwisha choka, alishatoka tayari,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Umri ukipinduka, myaka kuwa furifuri,
Mwili unanyang'anyika, hupatwa kila athari
Afya inabadilika, magonjwa huwatitiri,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Ndivyo ilivyomfika, hatima yake Amiri,
Amiri Sudi hakika, ndivyo alivyohajiri,
Jina likifahamika, Andanenga mashuhuri,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

"Sauti ya kiza" fika, lakabu yake Mahiri,
Ni Mtunzi msifika, atayedumu dahari,
Kwa miaka na mikaka, atabakia stori,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Kwa Sababu kaandika, vitabu vikadhihiri,
Tena vya kukubalika, kuuhusu ushairi,
Vichwani hatofutika, atabakia sanjari,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Kitabu chake fauka, kinachoitwa "bahari"
Soma utaelimika, kujua vina urari,
Pia nyingi kaziweka, aina za mashairi,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Mengi ya kustawika, kwenye hii Jamhuri,
Ya utunzi wa fanaka, wa juu kwenye mimbari
Kajenga hiyo twarika, nyayo zake tusawiri,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

Pia kwetu washirika, tumwombee kwa Kahari,
Mola mwenye mamlaka, pazuri amsitiri,
Apate kupumzika, peponi kwenye kasiri,
Kwenye chombo kaabiri, Andanenga kaondoka.

"Ni Mkonikoni wa washairi",
Abdallah Ahmed Seif (Ngome Imara),
0716 903355 - 0754 870196,
Dodoma.




***Amiri sudi Andanenga (Marehem)***

# Panya na Chura

Hapo zamani za kale aliishi Panya na Chura ambao walikuwa marafiki bora zaidi. Chura alipenda kuzungumza na rafiki yake panya hivi kwamba alikuwa akiruka kutoka kwenye kidimbwi chake kila asubuhi saa 8 asubuhi ili kutembelea nyumba ya rafiki yake panya.



Haikuwa nyumba kubwa. Lilikuwa ni shimo laini la ukubwa wa wastani kando ya mti umbali wa dakika 20 hivi. Wangezungumza kuhusu mada zinazovutia au za kuchekesha, wangepata kifungua kinywa pamoja na kufikia saa 11 asubuhi, chura angeaga na kuruka nyumbani.



Hakika panya alikuwa panya mwenye furaha sana. Alifurahishwa sana na ziara ya kila siku ya rafiki yake chura hivi kwamba hakujua kwamba rafiki yake alikuwa akizidi kumkasirikia kila mwezi uliokuwa ukipita. Chura alikuwa akigeuka polepole kuwa adui, zaidi ya kuwa rafiki wa karibu. Lakini panya hakujua kinachoendelea.



Kwa nini chura alizidi kukosa furaha, unaweza kuuliza? Kweli, chura aliumia kwa sababu ingawa alimtembelea panya kila siku, panya hakuwahi hata siku moja kutoa ofa ya kuja kumtembelea nyumbake. Hapana. Hata mara moja.

"Mbona Panya anasitasita kuja nyumbangu? Je, Panya anafikiri kwamba ninaishi katika nyumba yenye harufu mbaya? Je, nyumba yangu ni ya kiwango cha chini sana? Je, Panya anaona aibu kuonekana hadharani na mimi? Je, Panya anadhani sina senti na siwezi kumudu kumlisha?" Kulikuwa na maswali mengi sana yaliyokuwa yakiulizwa katika kichwa cha chura.

Siku moja, chura alihisi kwamba alikuwa amedhalilishwa vya kutosha. Kwa hiyo, wakati wa ziara ya siku hiyo, aliamua kufanya kitu kikali. Wakati wote wa kiamsha kinywa, chura alifunga ncha moja ya uzi kwa siri kwenye mguu wake na kwa ujanja akafunga ncha nyingine kwenye mkia wa panya. Na saa ilipopiga 11 AM, chura alisimama haraka na kuruka mbali, akiwakokota wanyonge na panya aliyeshtuka nyuma yake.

Punde, chura alifika kwenye bwawa lake na kuzama ndani yake. Panya alijaribu kujikomboa lakini hakuweza, na punde alizama kwa huzuni. Mwili wake maskini uliochoka ulielea juu.

Ndani ya dakika chache, mwewe mwenye misuli aliruka na kuona mwili wa panya uliokuwa ukielea juu ya uso unaometa wa bwawa. Mwewe alishuka chi kasi, akamshika panya kwenye makucha yake na kuruka hadi kwenye tawi la mti uliokuwa karibu. Chura, bila shaka, alitolewa nje ya maji pia! Alijaribu sana kujikomboa. Lakini alishindwa.



Mwewe hakuamini jinsi siku yake ilivyokuwa nzuri huku akicheka kimoyomoyo. Upesi alikomesha mapambano ya chura kwa kula chura kwa chakula cha jioni baada ya kula panya kwa chakula cha mchana.

Barani Afrika, wana msemo usemao: 'Usichimbe shimo lenye kina kirefu kwa ajili ya adui yako, unaweza kuanguka humo wewe mwenyewe'.

## Maadili ya Hadithi

1. Wafikirie wengine vizuri. Usifikirie mabaya zaidi kwa watu.

2. Ikiwa mtu hakukualika nyumbake, usikasirike. Toa visingizio fulao na uendelee. Ni sawa. Sio lazima uende kwenye nyumba za watu ili kufurahiya kuwa na kampuni yao.

3. Usiwe na hisia kupita kiasi. Usifikirie sana kwa nini mtu anafanya hivi na kwa nini mtu anafanya hivyo. Ikiwa sababu imefichwa na haionekani, labda ni busara zaidi kuiacha. Usiwe na shaka. Usipeleleze watu.

4. Ikiwa tuna hisia mbaya kuhusu nia ya mtu fulani ya kufanya tendo jema, labda tunapaswa kuliacha lipite. Hatuwezi kuona nia yake ambayo iko ndani kabisa ya moyo wake. Kwa hiyo, tusifikiri nia za kweli ni zipi. Mwenyezi Mungu pekee ndiye anajua.

5. Usimsikilize shaytan kama anavyopenda watu wanapochukia au kuoneana wivu au hata kukwepana. Kwa shayateen, watu waliogawanyika ni rahisi kushughulikia kuliko watu walioungana na lengo moja.

6. Ikiwa unaona kuwa kutembelea mtu kila siku inakuwa shida, unapaswa kuacha kuifanya. Au angalau, unapaswa kujaribu kumtembelea mara kwa mara. Kuwatembelea wengine kila siku kwa kawaida si wajibu, kwa hivyo huenda si lazima ufanye ziara hizi za kila siku. (Isipokuwa, kwa hakika, ikiwa una mzazi mgonjwa au ndugu wa karibu mgonjwa, basi, itabidi utathmini upya hali hiyo, in shaa Allah). Lakini kama sheria ya jumla, tembelea watu kwa wastani na tu ikiwa ni lazima. Na labda utafurahia kila ziara zaidi, inshaa-Allah.

## Hadithi:

Mtume[saw] amesema: "Jihadharini na dhana, kwani dhana ni hadithi za uwongo. Msitafute makosa, msifanyiane ujasusi, msigombane, msioneane kijicho, msichukiane, wala msijiepuke. Bali kuweni waja wa Mwenyezi Mungu kama ndugu."

Ṣaḥīḥ al-Bukhārī ٥٧١٩, Ṣaḥīḥ **Muslim** ٢٥٦٣

# NAHITAJI UNAPOTAKA KUPIKA COOKIES (Ingredients).

- UNGA- wowote wakawaida au ppf au wamchele
- SIAGI (prestige, blueband n.k) au MAFUTA
- SUKARI YOYOTE(nyeupe au brown)
- MAYAI( Sio kwa kila receipe)
- MAJI AU MAZIWA pia sio kwa kila receipe
- FLAVOUR Inategemea na aina ya cookie unayopika
- CUSTARD AU CORNFLOUR inasaidia cookies zako ziwe softvizuri na pia inaleta rangi nzur
- BAKINGPOWDER hii inatumika kwa kiasi kidogo sana pia sio lazima inasaidia cookies zako ziweze kuvimba kidogo nakukaa vizuri

Kwa mapishi zaidi ya Biscut.



# TANGAZO

## Tanziim ya Lajna Imaillah Tanzania

Taanzim ya lajna imaillah Tanzania inapenda kuwatangazia Lajna na Nasrat wote nchini kuwa Ijtmaa ya Lajna na Nasrat 2024 inatarajiwa kufanyika katika eneo la Jamaat Kitonga Dar es salaam tarehe 28 na 29 Juni 2024 ikifuatiwa na Shura siku ya Jumapili tarehe 30 Juni 2024 InshaAllah .

Hivyo Lajna na Nasrat wote wanakumbushwa kufanya maandalizi kwa ajili ya Ijtmaa yetu kama barua ya Ijtimaa inavyoelekeza. Pia wanakumbushwa kuchangia mchango wa Ijtimaa kiasi cha Shilingi 12,000/= kwa Lajna na 3,600/= kwa Nasrat. Allah atujaalie wote tuweze kushiriki ili kufanikisha Ijtmaa yetu InshaAllah

***Sadr Lajna Taifa***
***Zena Nyange.***

# HEKIMA YA DHABIHU

*Asemavyo Masihi aliyeahidiwa[as]*

Kutoka Uk> 01

zinazishinda zile dhabihu za nyimati za hapo kabla. Wingi wa dhabihu umefikia hadi kwamba uso wa ardhi umefunikwa na damu, hata kwamba kama damu zao zote zingekusanywa pamoja na kutaka kuzitiririsha, kwa yakini mifereji ingeanza kupita kwa hizo, na mito kutiririka, na maeneo yaliyo katika nyanda za chini na mabonde makubwa yangefurika na damu. Na kitendo hiki chahesabiwa katika dini yetu katika yale mambo yanayomsogeza mtu karibu na Mwenyezi Mungu."

***(Hotuba iliyofunguliwa, UK. 41)***

**NANI ATOE DHABIHU?**

Mtu mmoja alimwandikia barua Masihi Aliyeahidiwa[as] na kumuuliza kwamba mimi nilichangia kiasi cha pesa kidogo kwa ajili ya kutoa dhabihu ya pamoja lakini watu wengine waliniondoa kwenye wachangiaji kwa sababu mimi nilikuwa mwahamadiyya. Je, yafaa kwangu kutoa dhabihu nikitoa kiasi hiki cha pesa kwa ajili ya mchango wa sadaka hapo Qadian? Akasema:
"Dhabihu hutolewa kwa kuchinja mnyama na si kwa kutoa pesa katika mfuko wa mchango wa sadaka. ikiwa kiasi kile kinatosha basi toa dhabihu ya mbuzi mmoja, na kama hakitoshi na huna uwezo wa kuongeza basi si faradhi kwako kutoa dhabihu."

***(Gazeti la Badr, 14 Feb 1907)***

**KUSHIRIKIANA KATIKA KUTOA DHABIHU**

Mtu mmoja aliuliza swali kwamba je, inasihi kuchinja mnyama kama vile ng'ombe kwa kuchangia pesa kidogo kidogo pamoja na wasiokuwa waahmadiyya? Akasema:

"kuna haja gani ya kushirikiana na wasiokuwa waahmadiyya. kama kutoa dhabihu ni faradhi kwako basi unaweza kumchinja mbuzi na kama huna uwezo huu basi si lazima kwako kutoa dhabihu. hawa wasio kuwa wahmadiyya wanakuita kafiri hawapendi kushirikiana na wewe basi kwa nini unataka kushirikiana nao? mtegemee Mwenyezi Mungu."

***(Gazeti la Badr, 14 Feb 1907)***

**MNYAMA WA AINA GANI HUCHINJWA?**

Mtu mmoja alimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba kama hatupati mnyama ambaye anakidhi vigezo vilivyoelezwa katika Hadithi je, inasihi kumchinja mnyama mdogo? Akasema: Inafaa wakati kuna ulazima lakini siku hizi hakuna ulazima kama huu. Mtu anaweza kutafuta mapema kwani siku zinatosha, hivyo hairuhusiwi kutafuta njia au kuonesha uvivu bila sababu."

***(Gazeti la Badr, 23 Jan 1908)***

**KUFUNGA SAUMU SIKU YA IDUL ADH'HAA**

Khalifah tulmasihi wa pili[ra] akieleza kuhusiana na kufunga saumu siku ya idul-adh'haa na kufungua kwa kutumia nyama ya dhabihu anasema:

"Maulawii Muhammad Ibrahim wa Bakaa Pur aliniandikia kwamba itangazwe kuwa saumu inayofungwa siku ya Eid si sunna ya Mtume Muhammad[saw]. hii ilikuwa ni kawaida ya mtume muhammad saw kwamba alipokuwa na afya nzuri alianza kula kwa kutumia nyama ya dhabihu. hata hivyo hii si saumu kama vile mtu asipoifunga atakuwa amekosea. hii si saumu ya faradhi ni ya nafali na inasisitizwa kwamba anayeweza afunge kwa muda kidogo lakini ambaye ni mgonjwa mwingine asipoifunga si faradhi kwake wala hatapata dhambi. pamoja na hayo ikumbukwe kwamba si sahihi kusema kuwa saumu hii haipo kabisa katika sunna kama alivyoandika maulawii bakaa Puri. mimi niliwahi kumuona masihi aliyeahidiwa akitekeleza fundisho hili alipokuwa na afya nzuri. pia imezoeleka sana katika waislamu na haiko hivi bila sababu ni nafali inayosisitizwa na mtume muhammad sallallahu alayhi wa sallam alikuwa akiendelea kutekeleza jambo hili na atakayefanya hivi atapata thawabu lakini asipoweza hana dhambi."

***(Gazeti la Al Fazl, 17 Jan 1941)***

# MZEE SAIDI BAKARI SASAMKA KWA ALLAH AREJEA

**Na Mwana Historia wetu**

Bilal wa Alfadhal Tabora, miaka ya 90, msomaji mahiri wa Qur-an Tukufu, mtafiti anayetaka ushahidi, mwenye ghera na heshima kwa ukhalifa asiyekosa swala ya Ijumaa na kufika mapema, jazba na mahaba ya kuhubiri, kutanguliza dini mbele ya kila kitu. Sifa zote hizi ukizikusanya pamoja ndipo kwa usahihi unapata taswira ya mzee wetu BAKARI SASAMKA ambaye ametutoka jumapili asubuhi ya tarehe 12.05.2024 na kuzikwa alasiri siku hiyohiyo mjini Mwanza. Kwa hakika sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.

SAIDI BAKARI SASAMKA alizaliwa Uyui Tabora mwaka 1938. Wazazi wake walimpeleka Madrassa mwaka 1946. Jina zuri ni pambo la kujivunia. SASAMKA maana yake ni kuchangamka. Na kweli SAIDI alikuwa amechangamka toka utotoni. Ubongo wake wa kushika haraka ulimfanya apendwe na walimu chuoni. Kwa ile hofu waliyokuwa nayo wazazi wengi wa kiislam ya kwamba akipelekwa shule ataritadi wazazi wake hawakutaka kusikia hata kidogo jambo hilo la kumpeleka shule na hatimaye kumpoteza. Lakini Allah Ndiye mbora wa wapangaji.

Mwaka 1951 Baba yake alifariki na hivyo akawa anakwenda kwenye dirisha la darasa la shule na kusikiliza waliokuwa wanafundishwa darasani.
Na ikumbukwe huu ndio mtindo alioutumia MATHIAS MNYAMPALA na SIHIYANA SALEH MANDEVU kupata elimu. Siku moja Padri akamkuta anasikiliza pale dirishani na kwa upole akamuuliza unasubiri nini? SAIDI akamwambia alikuwa anafurahia hayo yaliyokuwa yanafundishwa darasani. Padri huyo akamwambia kesho aje kuanza shule na ikatokea ya kwamba aende moja kwa moja darasa la pili kwa sababu ya ubongo wake mkali na hivyo hakusoma darasa la kwanza na hiyo haswa ndio maana ya SASAMKA.
Akiwa shule ya Native Authority Sikonge alimaliza darasa la 4. Pale shuleni alikuwa mchezaji mzuri wa mpira wa miguu. Darasa la tano hadi la nane alikuwa KuzeHall Middle School.

Kama tulivyokwisha ona, SAIDI alikuwa na ubongo mkali na wala hakuwa tayari kupokea kila kitu bila ya kupeleleza na kufanya uchunguzi. Katika umri wake huo mdogo aliwapa masheikh wa kisunni wakati mgumu na maswali yake yalikuwa mawili, nyinyi mnasema Nabii Issa (A.s) amekwenda Mbinguni



*Mzee Saidi Bakari Sasamka*

hebu mniambie amekwenda kwendaje? Masheikh wakakaukiwa mate wasiwe na la kujibu bali kupiga Astaghfirullah nyingi naye SAIDI akawaambia Astaghfirullah sio jibu la swali langu. Swali jingine lililokuwa linamsumbua ni kuhusu hirizi kuziweka mlangoni ikiwa ni kinga. Hili lilimpa mashaka makubwa kwani licha ya kuweka hirizi mbu waliingia ndani na kusambaza malaria na masheikh hawakuwa na majibu isipokuwa kubaki vinywa wazi.

Mungu bariki mwaka 1963 mjini Tabora alikutana na masheikh wawili wa kiahmadiyya Sheikh INATULLAH AHMAD na Sheikh Rashid Sarwah. Mazungumzo yalienda hivi.
-Nyinyi ni dini gani?
-Sisi ni waislam
-Mnaamnini Nabii ISSA[as] yuko mbinguni?
-Hapana alikwishafariki zamani
-Naomba ushahidi
-Katika Kuruani Tukufu kuna aya nyingi zinathibitisha kifo cha Nabii Issa (a.s) katika sura 3 aya 60 Allah Anasema hali ya Isa ni sawa sawa na Adam. Allah anawalinganisha kwa sababu wote hatimae walikufa hakuna aliyepaa mbinguni. Sura 16:21:27 wale wote wanaoabudiwa na watu wamekufa. Sura 36 aya 69 tunayempa umri mrefu tunampindisha. Sura 3 aya 56 Allah anasema atamfisha kisha atamnyanyua kwake. Sisi tuna haki gani kubadili maneno ya Allah?

Kama tulivyokwisha ona ona SAIDI BAKARI SASAMKA alikuwa na ubongo mkali akawa ameelewa aya zilizotolewa na Maulamaa hao wa Jamati. Swali lake lingine lililokuwa linamsumbua
-Je mnatengeza hirizi?
-hiyo ni haramu katika Islam
-nipe taratibu za kujiunga
-akapatiwa Baiat na kuisoma
-Naomba nijiunge.
Mwaka 1963 SAIDI BAKARI SASAMKA akawa amejiunga toka wakati huo yakawa yametokea mabadiliko makubwa katika maisha yake.

Alipomaliza Shule akaajiriwa katika chama cha ushirika cha kuuza mazao na kujiunga na mashirika mengi ambapo alifanya kazi kwa bidii na uaminifu mkubwa. Wakati wote huo wa kuajiriwa aliendelea kuwa na mfungamano mkubwa na msikiti. Hakukosa sala na ndipo alipojipatia lakabu ya Bilal wa Al Fazl Tabora. Baadae alihamia Mwanza ambapo aliendelea kufungamana na Msikiti akiwa mstari wa mbele katika safari za kwenda kuhubiri nje ya Mwanza yaani Negezi, Bugumbagu, Kalenga, Kagongwa na sehemu nyingi za Shinyanga, Geita na Simiyu alifika kwa mahubiri. Umri haukuwa tatizo Kwake aliendelea kufikisha habari za ujaji wa Masih Aliyeahidiwa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (a.s)

Maisha ya Saidi Bakari Sasamka yanatuachia somo. Kutafuta elimu ni wajibu kwa kila Mwislamu ,SASAMKA alionesha mapenzi ya kutafuta elimu toka akiwa mdogo. Allah ametupatia akili na tunalazimika kuzitumia SAIDI BAKARI SASAMKA hakuwa mtu wa hewala bwana. Alitaka kujua na kupewa ushahidi. Maana ya maisha inakamilika unapokuwa na mfungamano na Ukhalifa. Mzee SASAMKA alikuwa karibu na msikiti na kutekeleza maagizo ya Khalifa ambayo siku zote anatukumbusha kufikisha ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa (a.s) kwa wengine. Jitihada kubwa alizifanya kutekeleza hayo.

Tunamuomba Allah apokee Juhudi zake nasi tulio baki tuchume jani kutoka katika mti wa maisha yake.
==========

***NB: Mwanahistoria wetu alikuwa na mazungumzo na Mzee SAIDI BAKARI SASAMKA-nyumbake Mwanza tarehe 14-07-2016.***

# HOTUBA YA EID UL ADHHA

*Kutoka Uk. 11*

tujitolee maisha yetu yote kwa Allah. Hili siyo suala la kutoa dhabihu fula muda mfupi bali ni kusimama imara katika kumtii Allah kwa namna hii ya kwamba mtu ajipoteze ndani mwake, kwa kumfanya Allah Mmiliki wa kila kitu na kujisalimisha mbele ya ridhaa Yake, huu ndiyo ujumbe inaotupatia Eid hii.(hotuba 28 sep 1982).
Pia Khalifa Mtukufu wa Nne wa Sayidna Ahmad as, Hazrat Mirza Tahir Ahmad akituelezea habari ya Eid ya kweli alisema "Jambo la mwisho ni hili ya kwamba muwawezeshe majirani zenu wenye hali ndogo, watu wasiojiweza na mafukara, washerehekee Eid ndipo mtaweza kusherehekea Eid ya kweli. Njia bora ya kutimiza mahitaji yenu ni kujishughulisha katika kuwatimizia mahitaji wengine. Muwahudumie maskini, muwatimizie mahitaji wenye shida na jifurahishe kuwafurahisha wengine na kumbukemba kutokana na watu hao, mnapewa riziki." (Hotuba 12 Feb 2003).
Naye Khalifa wetu mpendwa Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. anatuelezea namna ya kusherehekea Idi, kwa kusema: Eid yetu itakuwa idi ya kweli ikiwa hasa tutawajali watu wengine wenye matatizo. Si tu katika nchi yetu bali po pote kwingineko.
Mwenyezi Mungu Atusaidie sana kusherehekea eid kwa namna ambayo itakuwa ni yenye kutufikisha kwenye lengo hasa la maisha yetu, ambalo ni kumwabudu Mwenyezi Mungu kikamilifu. Amin.

# Kuendelea Utume Katika Umma wa Mtume Muhammad Sallalaho aleh wasallam.

**Ustadh Junaid Mbena**

Maombi ya Surat Alfatiha ni dalili kubwa kuendelea utume Alipotufundisha Allah tumuombee

اهدنا الصراط المستقيم .صراط الذين انعمت عليهم

Utuongoze kwenye njia iliyonyooka ,Njia ya wale uliowaneemesha

Mwenyezi Mungu akataja zile neema zilizotajwa katika Surat Alfatiha,lakini zilitajwa kwa Mujamalمُجْمَل
(kwa ujumla)
akataja katika Surat Nisa aya 69-70 katika njia ya Mubayyan مُبَيَّن
(kwa uwazi)

Wanazuoni wote wa sheria ya tafsiri wanasema

كُلُّ مُجْمَلٍ يَحْتَاجُ ٱلْمُبَيّنَ

Kila (aya) itakapokuja katika njia ya Mujmal
aya hiyo lazima itafutiwe kifafanuzi chake.

Aya hizi hizi mbili zinafafanuliwa ktk Sura Nisa 68-70 kwa ufasaha sana:
Aliposema Allah

Tafsiri ya sura Nisa 70_ _wanaotoa WAISLAMU WA JINA NI potovu kabisa_ _ambyo inapingana na Aya nyingi za Quran Tukufu kama wanaoyosema chini ya aya hii :_

**وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ**

_Na wote wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hao watakuwa pamoja na MITUME na maswiddiik na Mashahidi na watu salihina...._
Wanasema watiifu wa Mtume Muhammad SAW hawatapata daraja hizi dunia sababu (manabii,Masadiik mashahidi wala masalih)
hawatapatikana baada ya Mtume Muhammad SAW .

Na wanasema:
Waislamu ambao walitii au watatii wote hao siku ya Kiyama watakuwa pamoja na manabii ingawa watiifu hao hawakuwa manabii duniani na Pamoja na masadiik (waliopita ktk umma nyngine ) ingawa watiifu hao waislamu hawakuwa masadiik duniani na watakuwa pamoja na mashahiid(wa ummati wa mitume wengine) ingawa watiifu hao waislamu hawakuwa mashahid, na watakuwa pamoja na masalihi (watu wema waliopita kabla ya Muhammad SAW) ingawa watiifu hao waislamu hawakuwa masalih (watu wema) duniani.

kwa sababu Katika Aya hii Allah Aliunganisha vyeo hivi vyote pamoja,ukikataa "Annabiyyin" unabii utiifu baada ya Muhammad lazima ukatae vyeo vifuatavyo katika aya ile....
ndiyo wanavyofanya

**JIBU**

*Tunasema Tafsiri hii inaufedehesha utii wa Mtume Muhammad SAW Hali ya juu.*
*na kumtii yeye inalazmisha mtu apate cheo ktika dunia na Akhira awalau kimoja (kati ya vyeo vinne) sawa na Ucha Mungu wake.*

Na hata katika akhira sawa na tafsiri yao watiifu wa Mtume Muhammad SAW hawatapata vyeo hivi lakini watakuwa pamoja na waliowatii mitume wengine na walipata daraja hizi kabla ya Muhammad SAW.

Kwa sura hii waliotii mitume wengine watapata viti na vyeti vya Usadiik, ushahidi,usalih na waliotii Mtume Muhammad SAW watakuwa pamoja nao (kuangalia viti vyao au kuwalinda,je ???)

Kwa hiyo tafsiri hii ni potovu dhahiri na inafedhehesha daraja la utii wa Mtume Muhammad[saw] kweli kweli.
Waislamu wa jina hawana upendo wa Mtume Muhammad SAW hata kidogo wanapofanya tafsiri hii ili wafuate matamanio yao.

_Halafu waislamu wa jina wanasema_

**_ْفَأُولَٰئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِم_**

_" ULAAIKA" ismu ishara inafidisha "UMUUM"_
_kwahiyo maana yake ni "basi wooote hao watakuwa pamoja na wale walio neemeshwa na Allah_

_na baada ya maelezo haya wanasema tukikubali Tafsiri ya makadiani wote watakuwa miongoni mwa manabii kwa sababu ya neno Ulaaik_

**::::::JIBU:::::**

Faulaaik haifidishi kuwa wote hao watakuwa pamoja/miongoni mwa manabii ...
Kwa sababu:
Ukiangalia Sura Nisa 70. yenyewe inataja daraja nne za waaminio waliotii.

Kila mumin ana daraja lake la utii wa Mtume Mtukufu SAW
Utii wa Mtume Muhammad SAW unaweza kusababisha unabii utiifu wa Muhammad SAW , pia sawa na aya hii ina Alitaja madaraja mengine.
kutaja madaraja tafauti tafauti inagawa vyeo vya Watiifu sawa na Imani zao.
laki unabii tujue kwamba Nabii hatumwi ispokuwa uhitaji uwepo na mpango wa Allah kama uhitaji hamna, haji Mtume.
Kama alivyotubainishia wazi-wazi

**ۗاللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ**

[Surat Al-An'am 125]

"Mwenyezi Mungu anajua Atakapoweka utume wake."

kama waislamu hao wanaosema wote watakuwa pamoja na manabii,
(kwa sababu sawa na maelezo yao "Ulaaik" inafidisha wooote)
basi hakuna haja ya kugawa vyeo hivi vinne ,kila mtiifu atakuwa pamoja na manabii.

Halafu wanaposema watiifu wote wawe pamoja na mabii wote .
Tunajua kwamba Kila mumin hakuwa namna moja katika takwa ingawa alitii,lakini sawa na tafsiri yao hawa wote watakaa pamoja na manabii wote
Quran tukufu na Akili haikubali .

je,manabii hawana daraja katika pepo.????
Watakaa pamoja na watu ambao ni dhaiif sana ingawa waligofiriwa kwa sababu ya utii katika jambo maalum ????

Ina maana hakuna Jannat ya hali ya juu "Jannat ul firdoos"

Quran inasema kuhusu madaraja ya Mitume.

**تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۘ مِنْهُمْ مَنْ كَلَّمَ اللَّهُ ۖ وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ ۚ**

[Surat Albaqara 254]

Hao Mitume tumewafadhili badhi yao zaidi kuliko wengine.
miongoni mwao wako ambao Allah alisema nao sana na wengine wao akawapandisha daraja.

Na ukiangalia Quran hata kwa ajili ya waaminio wa kwaida ( Manabii ni habari nyingine) hawatakuwa daraja moja katika pepo.
kila moja atapata daraja lake sawa na imani yake.

**أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا ۚ لَهُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ)**

[Surat Al-Anfal 3]

"Hao ndiyo waaminio kweli kweli,wao wana vyeo kwa Mola wao."

Chini ya aya hii ya sura Anfaal wafasiri wa Quran wengi wanafafanua jambo hilo vizuri kwa mfano Katika Tafsir Ibn Kathir imeandikwa :

**جاء في الصحيحين أن رسول الله - صلى الله عليه وسلم - قال : إن أهل عليين ليراهم من أسفل منهم كما ترون الكوكب الغابر في أفق من آفاق السماء ، قالوا : يا رسول الله ، تلك منازل الأنبياء لا ينالها غيرهم ؟ فقال : بلى ، والذي نفسي بيده رجال آمنوا بالله وصدقوا المرسلين .**
**وفي الحديث الآخر الذي رواه الإمام أحمد [ و ]أهل السنن من حديث عطية ، عن أبي سعيد قال : قال رسول الله - صلى الله عليه وسلم - : إن أهل الجنة ليتراءون أهل الدرجات العلى كما ترون الكوكب الغابر في أفق السماء ، وإن أبا بكر وعمر منهم وأنعما .**

Tafsiri kwa ufupi:

Katika pepo watu wa daraja la juu watawaona watu ambao ni daraja la chini kama mnavyoona nyota za kilimia katika mbingu.

(Hadithi hii imekuja katika Bukhari na Muslim)

Na katika Hadithi nyingine imeambiwa madhmuni hii hii lakini alisema mnamo Abubakar na Umar R.A.

Na Imam Tibri analeta Maelezo chini ya Aya hii kwamba hizi daraja za Jannah ni 70.

**لهم درجات عند ربهم "، قال: الدرجات " : سبعون درجة, كل درجة حُضْر الفرس الجواد المضمَّر سبعين سنة.**

Daraja zipo 70
kila daraja ni umbali wa mwendo wa farasi aliyeandaliwa kwa Safari kukimbia miaka 70

*Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo*

# HOTUBA YA EID UL ADHHA

*Kutoka 12..*

Kwa mujibu wa Falsafa ya Islam Eid huja baada ya mwaminio kujitolea muhanga mkubwa au dhabihu kubwa kwa ajili ya Mola wake. Kwa mfano Eid ul Fitri inasherehekewa baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhani ambamo huwa tunajitoa dhabihu kwa namna mbalimbali kwa ajili ya Allah na hisia zetu zote tano, zinashiriki katika dhabihu hizo. Tunajizuia mchana kutwa na kula na kunywa pamoja na starehe zingine zote ambazo katika siku zingine zinakuwa ni ruhusa.

2

Eid tunayoisherehekea leo inatuhimiza na kututaka tujitolee dhabihu maisha yetu yote kwa Allah, kwa kutukumbusha dhabihu ya familia moja ya watu watawa na wachamungu sana ambao waliyatoa maisha yao yote kwa ajili ya Allah Mwenye Enzi. Familia hiyo ni ya Nabii Ibahim[as]. akiwa yeye na mke wake Bibi Hajira[ra]. na mtoto wao Nabii Ismail[as].

Nabii Ibrahimu[as]. na familia yake walijitolea muhanga na dhabihu kwa kiwango cha hali ya juu sana kiasi hiki kwamba ibada yote ya Hija na sikukuu ya Eid ul Adhha ni mkusanyiko wa matukio na matendo mbalimbali waliyoyafanya katika kujitolea kwao mbele ya Mwenyezi Mungu. Ibada ya Hajj ambayo hufuatiwa na sikukuu hii ya Kuchinja au Eidul Adh'ha kwa ujumla imesheheni matukio na matendo hayo mbalimbali aliyoyafanya Nabii Ibrahim[as] na familia yake na yamefaradhishwa kwetu ili tuweze kujifunza hekima zake.

Nabii Ibrahimu[as] alijaribiwa kwa amri mbalimbali lakini yote akayashinda, kama asemavyo Allah:

Na kumbukeni Mola wake Alipomjaribu Ibrahimu kwa maneno, basi akayatimiza

katika majaribu yote, yako mawili yenye kusisimua sana moyo na kuyafanya macho yabubujikwe na machozi, huku roho ikipata matumaini makubwa kwamba kweli Mungu yu pamoja na wamchao.

Jaribio la kwanza ni pale Nabii Ibrahimu kwa agizo la Kimbingu alipotakiwa kuipeleka na kuiacha familia yake ya watu wawili tu (Mke na mtoto) katika bonde lililopo jangwani, lisilokuwa na kitu, lisilokuwa na miti ya matunda, lisilokuwa na maji bali lisilokuwa na wakazi wowote wa kudumu zaidi ya wapita njia wa msimu kwa msimu. Kikubwa kilichokuwepo hapo ni msingi wa zamani wa nyumba ya kwanza kujengwa kwa ajili ya Ibada ya Mungu Mmoja.

Basi kwa kutimiza agizo hilo la Mola Wake, Nabii Ibrahimu[as] akawachukua mke wake bibi Hajira[ra] na mtoto wake Ismail katika safari ndefu, ambayo yumkini ilikuwa ya miguu hadi walipofika mahala alipoagizwa. Hapo akiwakabidhi mfuko mdogo wa tende na kiriba kidogo cha maji akawaambia ninawaacheni hapa nami naondoka. Kwa kusema hayo, Nabii Ibrahimu[as] akainuka na bila kutazama nyuma akaanza safari, huku Bibi Hajira[ra] akibaki amepigwa na butwaa kwa kile kinachoendelea mbele ya macho yake.

Bibi Hajira[ra] katika hali ya taharuki akamuuliza Nabii Ibrahimu[as], je ni kweli unatuwacha, ni kweli unatuwacha, ni kweli unatuwacha hapa? lakini Nabii Ibrahimu[as] hakugeuka kutazama nyuma. Hatimae akamuuliza, Je, kutuacha huku ni matamanio yako tu, au ni amri ya Mwenyezi Mungu? Hapo Nabii Ibrahimu[as] akageuka na kumjibu mkewe, hii ni Amri ya Allah. Kusikia hivyo bibi, Hajira[ra] kwa ujasiri mkubwa na kwa kumtegemea Allah, akasema, kama hii ni Amri ya Allah, basi Allah hatotuacha.

Basi Nabii Ibrahimu[as] akapotea kwenye macho ya bibi Hajira[ra], na haukupita, muda kwa joto kali na kavu la jangwani, maji ambayo bibi Hajira[ra] aliyakusudia yawe ya mtoto wake tu, nayo yakaisha na muda si mrefu mtoto akaanza kuhangaika kwa kiu ya jangwani.

Hapo Bibi Hajira[ra] akapata fadhaa kubwa, je itakuwaje hali yao kama hawakupata msaada angalau wa maji. Katika hali hiyo, kana kwamba hakutaka kumuona mtoto wake akifariki mbele ya macho yake akaanza kukimbia baina ya vilima viwili vilivyokuwepo karibu na walipoachwa. Vilima vya Safa na Marwa, huku akiangaza huku na kule kila alipofika juu ya kila kilima kwa matarajio ya kumuona angalau mpita njia atakayeweza kuwasaidia maji ya kunywa. Alifanya hivyo, akipanda na kushuka kwa mara saba na mwishowe akiwa amechoka, ama kwa kupata ilham, akarejea alipomlaza mwanawe na tahamaki maji yalikuwa yanabubujika miguuni mwa mtoto wake.

Allah akababujisha chemchem ya zamzam ambayo ikawa sababu ya wao kupata mustakbali wa kuishi hapo na watu wengine kukusanyika hapo hadi leo.

Tukio la pili lililo na ukubwa kama la kwanza au zaidi ni pale Nabii Ibrahimu[as] alipotakiwa kumtoa dhabihu mwanawe wa pekee mara tu alipofikia baleghe.

Allah analielezea kwa uzuri mno jaribio hili katika aya tulizozisoma mwanzoni, ya kwamba: ...

Hivyo maadhimisho ya Idi hii ya dhabihu yanayo hekima kubwa na hapa chini nitanukuu baadhi ya maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na makhalifa wake mbalimbali jinsi wanavyotutarajia tulielewe jambo hili.

Mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya waislamu waahmadiyya, Hazrat Ahmad[as], Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa alisema "Mtu anapaswa kuwa mkweli na mwaminifu kama Hazrat Ibrahimu[as] aliyekuwa tayari kumchinja mwanaye. Vilevile mtu hawezi kuwa chochote mpaka aachane na matamanio yake yote ya kidunia. Mimi nasema kweli kwamba mtu anapomwamini Allah na kujaaliwa jazba fulani kutoka Kwake hapo Allah Huwa Msaidizi na Mlinzi wake". (Malfudhaat , Jalada 4 , Uk 243 )

Sayidna Ahmad as akielezea njia ya kupata ukaribu na Allah alisema "Njia ya kupata ukaribu na Allah ni hii ya kwamba mtu aoneshe ukweli kwa ajili Yake. Sababu ya Hazrat Ibrahimu as kupata ukaribu na Allah ilikuwa ni hii ya kwamba yeye alisikia sauti isemayo:

"Na Ibrahimu aliyetimiza ahadi" wakati alipokuwa tayari kumchinja mwanaye.

4

Mwenyezi Mungu Hutazama matendo na kuridhika nayo. Na matendo hutokana na huzuni lakini mtu anapokuwa tayari kupata huzuni na taabu kwa ajili ya Allah basi Allah Hamtii mtu huyo katika huzuni na taabu. Tazamemba Hazrat Ibrahimu a.s. alipotaka kumchinja mwanaye na kufanya matayarisho yote kwa ajili ya kuitii amri ya Mwenyezi Mungu basi Mungu Akamwokoa mwanaye." (Malfodhaat, Jalada 2, Uku 704).

Pia Hazrat Masihe Mauud as alisema: "Nyama na damu sio dhabihu ya kweli bali Kuzitakasa nyoyo ndiyo dhabihu ya kweli. Watu wa kawaida huwachinja wanyama tu lakini watu makhsusi huzichinja nyoyo zao. Mwenyezi Mungu Hakukataza kutoa dhabihu ya wanyama ili kuonesha kwamba dhabihu hizi pia zinamhusu mtu." (Barahine Ahmadiyya, Ruhani Khazain Jalada 21 Uk 424).

Khalifa Mtukufu wa Kwanza wa Sayidna Ahmad[as], Hazrat Maulvi Hakim Nurud din[ra], akibainisha falsafa ya dhabihu alisema "Kujitolea ni kazi ngumu sana. Tazamemba kulikuwa na vikwazo vingi pindi dhabihu hii ilipoanza kutolewa. Hazrat Ibrahimu a.s. alikuwa mzee sana, mwenye umri wa miaka 99 na mwenye afya isiyo nzuri. Lakini Mwenyezi Mungu, sawa na ahadi Yake, alimjaalia Hazrat Ibrahimu[as], mtoto kama Ismaili na Hazrat Ismaili alipokua, ikatoka amri ya kwamba Ismaili atolewe dhabihu. Sasa angalieni dhabihu ya Hazrat Ibrahimu as ! alikuwa na umri wa miaka 99 na katika umri huo na uzee huo hakukuwa na matarajio na nguvu ya kupata tena mtoto. Lakini Hazrat Ibrahimu[as] aliachana kabisa na mipango na matamanio yake yote kiasi hiki kwamba alipopata amri, mara moja akadhamiria kumtoa dhabihu mwanaye. Sasa Mwana huyu pia alikuwa ni mwema kiasi gani ya kwamba Hazrat Ibrahimu[as] alipomwambia tu: "Ewe Mwanangu, hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja, basi fikiri waonaje?" Hapo mwana huyo mwema akajibu mara moja bila wasiwasi wowote "Ee Baba yangu, fanya unayoamriwa, utanikuta Inshallah miongoni mwa wanaosubiri" waila angeweza kusema kwamba hii ni ndoto tu ambayo inaweza kufasiriwa lakini hakusema neno la namna hii. Ilimuradi, baba na mwana, wote wawili wakaonesha utii wa hali ya juu na hawakubakiza heshima, raha, mali na matamanio yoyote. Na dhabihu zetu za leo ni mfano wa dhabihu hiyo Tukufu."

Naye Khalifa Mtukufu wa pili wa Sayedna Ahmad as, Hazrat Muslehe Mauud[ra] alisema "Basi Eid hii ni yenye shani kubwa sana ambayo hakuna mfano wake duniani kote. Katika Eid hii, waislamu huchinja mbuzi, ngombe na kadhalika lakini Qurani Tukufu Inasema:

"Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao lakini unamfikia Utawa wenu" (sura 22 aya 38) yaani nyama na damu za dhabihu hizi, hazimfikii Allah bali ni ucha Mungu wa watoao dhabihu unaomfikia Allah. Hivyo basi, dhabihu ya kweli ni dhabihu ya nafsi ya mtu na wanafamilia wake (anayoitoa kwa ajili ya Allah) na hili ndilo soma

5

inalotufundisha Eid ul Azhaa. Tazamemba Hazrat Ibrahimu aliwaacha Hazrat Hajira ra na Hazrat Ismaili as katika pori lisilo na maji wala matunda ..... na hii ilikuwa ni dhabihu ya familia yake yote. Ninaamini ya kwamba leo, kama kila mwislamu aanze kusherehekea Eid yake kwa maana hiyo ya kwamba pamoja na kuchinja mbuzi, ngombe na kadhalika, atoe dhabihu ya nafsi yake na watoto wake basi hakuna nguvu yoyote ya kidunia inayoweza kuwaangamiza waislamu. (hotuba 19 July 1956).

Khalifa Mtukufu wa Nne wa Sayedna Ahmad as, Hazrat Mirza Tahir Ahmad rh akieleza hekima ya kuisherehekea Eid kubwa alisema "Njia za kiislamu za kusherehekea sherehe mbalimbali ni tofauti kabisa na njia za dini zingine zote. Tofauti hiyo ni ya aina mbalimbali lakini leo nimechagua aina fulani ya tofauti kwa ajili ya kubainisha maelezo yangu. Katika Uislamu, hekima iliyofichikana ya kuadhimisha sherehe yoyote ni tofauti na sherehe zingine (za kidunia). Kama tujuavyo sote kuwa kwanza tunasherehekea Eid ul Fitri ambayo inasherehekewa baada ya mwezi wa Ramadhani uliojaa shida. Huwa tunatoa dhabihu ya namna mbalimbali kwa ajili ya Allah (katika mwezi huo) na hisia zetu zote tano, zinashiriki katika dhabihu hizi basi Eid hiyo huitwa Eid ul Fitri ambayo tulikuwa tukiipa jina la "Eid Ndogo" utotoni mwetu lakini leo tumejumuika kusherehekea Eid ul Azhaa inayoitwa pia Eid ya dhabihu na tulipokuwa watoto tulikuwa tukiiita "Eid Kubwa". Ikichunguzwa kidogo itabainika ya kwamba yeyote aliyetoa majina haya (ya Eidi hizi mbili), ametoa sawasawa kabisa. Kwani dhabihu tunazozitoa wakati wa Eid ul Fitri ni ndogo sana na za kwaida kuliko dhabihu zitolewazo wakati wa Eid ul Azhaa. Eid tunayoisherehekea leo inatuhimiza na kututaka

*Ukurasa 09*

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

# Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

## Mzee Saidi Bakari Sasamka kwa Allah Karejea

HABARI UK> 09



KWAHERI ANDANENGA

*Uk. 06*

HABARI UK> 8

## TANGAZO

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah Tanzania

# HOTUBA YA EID UL ADHHA

HABARI UK> 11




فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ السَّعْيَ قَالَ يٰبُنَيَّ اِنِّيْٓ
اَرٰى فِي الْمَنَامِ اَنِّيْٓ اَذْبَحُكَ فَانْظُرْ
مَاذَا تَرٰى ؕ قَالَ يٰٓاَبَتِ افْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۫
سَتَجِدُنِيْٓ اِنْ شَآءَ اللّٰهُ مِنَ الصّٰبِرِيْنَ ﴿۱۰۳﴾
فَلَمَّآ اَسْلَمَا وَتَلَّهٗ لِلْجَبِيْنِ ﴿۱۰۴﴾ ۚ
وَنَادَيْنٰهُ اَنْ يّٰٓاِبْرٰهِيْمُ ﴿۱۰۵﴾ ۙ
قَدْ صَدَّقْتَ الرُّءْيَا ۚ اِنَّا كَذٰلِكَ نَجْزِي
الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۱۰۶﴾
اِنَّ هٰذَا لَهُوَ الْبَلٰٓؤُا الْمُبِيْنُ ﴿۱۰۷﴾
وَفَدَيْنٰهُ بِذِبْحٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۰۸﴾
وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِي الْاٰخِرِيْنَ ﴿۱۰۹﴾ ۖ
سَلٰمٌ عَلٰٓى اِبْرٰهِيْمَ ﴿۱۱۰﴾
كَذٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِيْنَ ﴿۱۱۱﴾

103. Basi alipofikia umri wa kuweza kukimbia na kutembea naye, akamwambia: Ewe mwanangu, hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja, basi fikiri waonaje? Akasema: Ee baba yangu! Fanya unayoamriwa, utanikuta inshallah miongoni mwa wanaosubiri.

104. Basi wote wawili waliporidhika na akamlaza kifudifudi.

105. Mara Tukamwita: Ewe Ibrahimu!

106. Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyo Tuwalipavyo watendao mema.

107. Bila shaka (jambo) hili ni jaribio la bayana.

108. Na Tukamkomboa kwa dhabihu kubwa.


109. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye,

110. Amani iwe kwa Ibrahimu.

111. Hivi ndivyo Tunavyowalipa watendao wema.

Sura 37 aya 103 hadi 111

Kwa fadhili za Allah Mwenye Enzi leo tunasherehekea sikukuu ya Eid ul Adhha. Eid ni ile furaha au maadhimisho ambayo huja na kujirudia tena baada ya muda fulani. Hivyo Eid ul Adhha ni sikukuu ambayo huja baada ya kumalizika kwa ibada ya Hijja ambayo ni nguzo ya tano katika nguzo za Kiislam. Hata hivyo Eid hii huitwa Eid ul Adhha kwa maana ya Eid ya kuchinja au Idi ya dhabihu.



JESUS' ATONEMENT
(Swahili Translation)


This book was first written in English by Dr. Mufti Muhammad Sadiq r.a., the first Ahmadiyya Missionary in America.

The book discusses shortly but precisely on the following topics:

**The need for Atonement**
**Disapproval of Atonement theory**
**Historical facts about Atonment**
**Why we are rejecting Atonment**
**The origin of Atonment**
**How to get rid of Sins**

We hope that the book will benefit those who will read it thoughtful

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT
TANZANIA



KAFARA
YA
YESU

DR. MUFTI MUHAMMAD SADIQ R.A.

JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA TANZANIA

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 950/=

## Je, Wajua?

Je wajua kuwa ili uone kitu, basi mwanga unaotoka katika kile kitu unatakiwa uwe umefika machoko. Mwanga wa jua unatumia dakika nane kufika duniani. Mwanga wa nyota unachukua miaka milioni kadhaa kufika duniani. Hivyo uonapo nyota, fahamu kwamba unachokiona hasa ni mwanga uliotoka katika nyota miaka milioni iliyopita, na unafika katika macho yako muda huo unaoangalia. Unachokiona sio sasa, unaona historia. Wanasayansi wanatumia historia hiyo kujua dunia iliumbwaje.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com